

Familia zinahitaji kujua nini kuhusu Muundo Jumuishi wa Kujifunza (UDL)?

Kanuni za Muundo Jumuishi wa Kujifunza (UDL) ambazo familia zinapaswa kujua:

- ✓ Tuundo Jumuishi wa Kujifunza ni mfumo wa kupanga unaoweza kutumika katika ngazi zote za elimu na kuzalisha mtaala mnyumbu, wazi na unaoweza kukidhi mahitaji ya wote.
- ✓ UDL ni mbinu ya kupanga ambayo inaunga mkono ujumuishaji lakini si zana pekee inayohitajika ili kufanikisha elimu jumuishi.
- ✓ UDL inatambua kwamba hakuna njia moja ya kujifunza, na kwa hiyo, hakupaswi kuwa na njia moja ya kufundisha. Aina tofauti za motisha, uwakilishi, na kujieleza, zinapaswa kuwezeshwa (kanuni 3).
- ✓ UDL inamaanisha kuwa tunazingatia uwezo wala si ulemavu, inatuambia kwamba hatupaswi kuwaweka wanafunzi katika vikundi fulani kwa njia isiyofaa.
- ✓ UDL inathamini utofauti unaopatikana katika kila darasa, inapanga ikizingatia utofauti huo na inatupilia mbali mbinu ya kuzingatia mapungufu na badala yake inazingatia ujuzi.
- ✓ UDL inatambua kuwa kinacholemaza ni muktadha wala si watu.

Jumbe muhimu ambazo familia zinaweza kuendeleza:

- ✓ UDL inaendeleza mtindo wa kujifunza unaozingatia watoto wote.
- ✓ Msingi wa UDL ni kwamba walimu lazima wafahamu kikundi chao chote cha wanafunzi. Kwa njia hiyo, kila moja ya shughuli za madarasa inapangwa kulingana na utofauti wa wanafunzi, vizuizi vya mazingira vinatambuliwa na mipango ya kukabiliana navyo inafanywa, maarifa ya hapo awali ya wanafunzi yanaendelezwa, na vifaa mbalimbali na mikakati ya kufundisha inatumwa ili kila mtu aweze kushiriki katika mchakato wa kujifunza.
- ✓ Inatambulika pia kuwa baadhi ya wanafunzi wanaweza kuhitaji marekebisho fulani yatekelezwe ili washiriki. Marekebisho yanayowezekana lazima yatekelezwe katika hali zingine hata kama UDL inatumwa.
- ✓ Utumiaji wa UDL haimaanishi kuwa wanafunzi wote wajifunze maudhui sawa, badala yake kila mmoja apige hatua mbele katika mchakato wao wa kujifunza kwa kushiriki katika mchakato sawa wa kujifunza.
- ✓ UDL sio mbinu mahususi kwa wanafunzi wenye ulemavu ambao wako katika mfumo wa kawaida, ni mbinu ya kupanga ambayo hutoa majibu kwa hali ya utofauti darasani, ni mbinu ambapo ufahamu wa mwalimu kuhusu wanafunzi ni muhimu.
- na mguso. Kila hisia inapaswa kuchochewa ili mwali muu aweze kuchochea maendeleo na kujifunza katika kikundi chao cha darasa.
- ✓ Katika muundo huu, watoto hawatathminiwi kwa njia ile ile, yaani, wawulana na wasichana hawalinganishwi kwa kuzingatia jinsi wengine wanavyojifunza, bali kwa kuzingatia maendeleo yao wenyewe katika kujifunza.
- ✓ UDL hutumia mbinu ya kuzingatia fani mbalimbali inayohusisha masomo tofauti yanayoshughulikia mada ile ile na hiyo hupunguza mzigo wa masomo na kufanya kujifunza kuwe na ufanisi na maana zaidi.
- ✓ Walimu wengi huhusisha familia katika miundo yao. Hiyo ni bora kwa sababu maarifa yanayotolewa na wanafamilia huboresha mchakato wa kufundishwa kwa ajili ya watoto wote.
- ✓ UDL sio mbinu mahususi kwa wanafunzi wenye ulemavu ambao wako katika mfumo wa kawaida, ni mbinu ya kupanga ambayo hutoa majibu kwa hali ya utofauti darasani, ni mbinu ambapo ufahamu wa mwalimu kuhusu wanafunzi ni muhimu.